**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA**
**MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI WA MBULU**
**SHULE YA SEKONDARI CHIEF SARWATT**

Ofisi ya Mkuu wa Shule,
S. L. P 42,
**Mbulu – Manyara.**

**Kumb Na.SSS/F05/01/VOL2**

SIMU: +255 684-087292/0768-853245 (Mkuu wa shule)
+255 0786-568975 (Makamu Mkuu wa shule)
Email: ***ramlaibrahim3245@gmail.com***

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

S.L.P…… .

……

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHIEF SARWATT**

**HALMASHAURI YA MJI WA MBULU MKOA WA MANYARA MWAKA 2022/2023**

1. Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii kwa mwaka **2022/2023** tahasusi ya **PCB/PCM/CBG**. Shule ya sekondari **CHIEF SARWATT** ipo kata ya Endagikot umbali wa kilomita tatu (03) kutoka Makao makuu ya Halmashauri ya Mji wa Mbulu. Shule itafunguliwa tarehe _____kuanza masomo kwa muhula wa kwanza

- Kwa usafiri wa Mbulu,

**(i)** Magari madogo aina ya land **cruiser kutoka** Arusha kupitia Magara au Karatu – Mbulu/ au

(ii) Basi kubwa la SUNVIC **kutoka** Arusha – Mbulu.

(iii). Basi la **JESUS LOVE** kutoka Singida hadi Mbulu na mengineyo.

(iv) Magari madogo aina ya Land Cruiser kutoka Arusha hadi Mbulu

(v)Magari makubwa na madogo aina ya land Cruiser kutoka Babati hadi Mbulu

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia**

**2.1 Sare ya Shule**

(a) Mwanafunzi anatakiwa ajishonee sare za shule kwa kufuata maelekezo ya mashono kama ilivyo kwenye mchoro ulioambatishwa. Pia rangi ya kitambaa kimeambatishwa na fomu hii, kitambaa kinatakiwa kiwe kizito (namba moja).

– **SARE KWA WASICHANA**

Mshono wa sketi zote za darasani na kazi uwe kama unavyoonekana hapa chini.

**WASICHANA**

(i) Sare ya shule hii ni sketi na shati la mikono mirefu kwa wasichana yenye rangi ya **Bluu bahari pea** mbili-utajishonea

(ii) Shati nyeupe la mikono mirefu pea mbili-utajinunulia

(iii) Tai ndefu bluu bahari yenye mchirizi mmoja mweupe kama ilivyoonyeshwa kwenye mchoro kwa wavulana na wasichana-utajishonea

(iv) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na gidamu visivyo na visigino virefu vyenye kufunika mguu wote pea mbili (2) kwa ajili ya darasani.

(v) Soksi jozi nne nyeupe.

(vi) Sweta moja lenye rangi ya Sketi-utakuja nalo

*****Tafadhali shona rangi ya Light Blue (Blue Bahari)

* Sketi inapaswa kushonwa sentimita 30 kutoka kwenye goti kwenda chini-**Matron atakagua**.

**SARE KWA WAVULANA**

(i) Suruali rangi ya bluu bahari pea mbili yenye pindo nne kwa mbele kama mchoro unavyoonyesha (Celebration)– utajishonea

(ii) Shati jeupe la mikono mirefu – utajishonea

(iii) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na gidamu visivyo na visigino virefu vyenye kufunika miguu yote pea mbili (2) kwa ajili ya darasani.

(iv) Soksi jozi nne nyeupe.

(v) Sweta moja lenye rangi ya Suruali – utakuja nalo.

*NB: Suruali za mlegezo (chupa) haziruhusiwi shuleni*

**SARE ZA SHULE KWA WANAFUNZI WA KIISLAMU**

Wasichana wa madhehebu ya kiislamu wanapaswa kuvaa "HIJABU" (kijuba)
kulingana na maadili ya dini yao na si vinginevyo

1. Suruali rangi ya bluu bahari pea mbili yenye pindo nne kwa mbele kama mchoro unavyoonyesha (Celebration)–utajishonea
2. "S h o r t" Kanzu mbili nyeupe nchi 12 kutoka chini na isiyo na mipasuo pembeni zenye mikono mirefu na "**HIJABU" NYEUPE ISIYO NA UREMBO WA AINA YOYOTE** – Utajishonea.
3. Kinyume na maelezo ya mashono hutapokelewa

NB:

1. *Mwanafunzi hataruhusiwa kuja na nguo za nyumbani bali aje na vitu alivyoagizwa tu.*
2. *Siku ya kuripoti aje akiwa amevaa sare sahihi za shule*
3. Uvaaji wa sare ya shule ni muhimu na ni lazima uwe na sare ya shule yenye heshima na utakaguliwa ufikapo shuleni kama tunavyoagiza katika fomu hii

**Sare ya Michezo kwa Shule hii ni**

i. Track ya light blue na mistari meupe- utakuja nayo (Ni lazima kwa wanafunzi wote)
ii. Raba pea moja (1) nyeusi.

**Vazi la kazi**

(i) Sketi mbili dark blue nzito mshono kama sketi za darasani
(ii) Suruali mbili dark blue mshono kama suruali za darasani
(iii) Raba/sendo (mwanafunzi haruhusiwi kuvaa ndala nje ya bweni, darasani ama bwaloni)
(iv) Vazi la kazi litavaliwa na T-shirt yenye nembo ya shule ambayo inapatikana shuleni kwa Tsh. 12,000/= tu.
(v) Kila mwanafunzi aje na pull-neck mbili nyeupe kwa ajili ya kujikinga na baridi

**2.2 Ada na michango ya shule**

**a)** Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= kwa mwanafunzi wa bweni. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000/= kwa mwanafunzi wa bweni kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule Benki ya **NMB kwa Ac. 41201200074**, jina la Akaunti ni CHIEF SARWATT Sec. School Recurrent Account. Unapofika shuleni unapaswa kuwasilisha "Bank – pay in slip" kwa mhasibu wa shule. (*tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip*)

**b)** Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni; -

**ADA NA MICHANGO**

| S/N | FEDHA | MWAKA | MUHULA I | MUHULA II | MAONI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ada ya shule kwa mwaka | 70,000/= | 35,000/= | 35,000/= | |
| 2 | Grarama ya tahadhari (hairudishwi) | 5,000/= | 5,000/= | 5,000/= | |
| 3 | Kitambulisho na Passport siza (Picha_ | 5,000/= | 6,000/= | | |
| 4 | Nembo | 3,000/= | 5,000/= | | |
| 5 | Uboreshaji wa Taaluma kwa mwaka | 20,000/= | 10,000/= | 10,000/= | |
| 6 | Ulinzi | 20,000/= | 10,000/= | 10,000/= | |
| 7 | Huduma ya kwanza hapa shuleni na Usafiri wa wagonjwa | 10,000/= | 5,000/= | 5,000/= | |
| 8 | Mahafali ya kidato cha Nne na Sita | 5,000/= | 5,000/= | 5,000/= | |
| 9 | Mpishi | 20,000/= | 10,000/= | 10,000/= | |
| 10 | Ukarabati wa samani | 10,000/= | 10,000/= | 5,000/= | |
| 11 | Mitihani ya kujipima | 20,000/= | 10,000/= | 10,000/= | |
| | | 188,000/= | | | |

**NB:** Wanafunzi wanashauriwa kujiunga na mfuko wa bima ya afya ICHF ambapo bima kubwa ni Ths. 50,000 na anaweza kutibiwa hospitali ya Wilaya pamoja na hospitali ya Haydom. Pia anaweza kulipa Tsh. 6,000 shuleni alafu watajiunga wanafunzi watano na itatumika kwa matibabu katika hospitali ya Wilaya tu. Hivyo kila mzazi anatakiwa amlete mwanafuzi shuleni akiwa na Bima ya Afya.

**Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni; -**

i. Unashauriwa kuja na vitabu vya masomo ya tahasusi/(combination) yako
ii. Ndoo mbili (3) zenye ujazo wa lita 10 kwa matumizi binafsi na zenye mifuniko kwa ajili ya usafi.
iii. Madaftari (counter books) na kalamu za kutosha
iv. Rula na mathematical set.
v. Scientific calculator (Non Programmable)
(vi) RIM moja (1) size A4 na RULLED (1) kwa muhula.
vi. Mwavuli mmoja ambao utatumia wakati wa mvua.
vii. Kuna baridi hivyo mzazi anashauriwa amnunulie mwanafunzi Track suit pea 1 kwa ajili ya kuvaa usiku wakati wa kujisomea- Rangi ya kijivu utakuja nayo.

## Vifaa vya bwenini

i. Mto mmoja (1) na foronya mbili za rangi ya pink kwa wasichana na bluu bahari kwa wavulana.
ii. Chandarua/neti ya mstatili kwa kuzuia mbu –(rangi NYEUPE), Blanket moja (1) nzito, Taulo moja (1), night dress, shuka pea mbili rangi ya blue bahari kwa wavulana na pink kwa wasichana.
iii. Godoro utalikuja nalo size2 $\frac{1}{2}$
iv. Sanduku la bati/chuma la kufunga kwa kufuli imara.

v. Pazia moja la rangi ya light blue kwa wavulana na rangi nyeupe kwa wasichana, utatunza mwenyewe na kuondoka nalo ukihitimu shule.
vi. Kanga doti moja kwa wasichana kwa kuogea tu na ndala kwa wanafunzi wote
vii. Dawa ya meno, mswaki na mafuta ya kujipaka (Haruhusiwi kutumia vipodozi vya aina na mapambo)

**VIFAA VYA USAFI**

- **PCB**- Squeezer, Slasher lililonolewa vizuri na brush ya kusugulia sink
- PCM- Squeezer, Slasher lililonolewa vizuri na fagio wa chelewa
- CBG- Squeezer, jembe jipya lenye mpini imara na fagio wa chelewa

*NB: kila mwanafunzi aje na sh. 5,000/= kwa ajili ya kununulia dawa ya chooni*

Vyombo vya chakula

- Sahani ya bati (Aluminium) moja
- Bakuli la bati(Aluminium) moja
- Kijiko na kikombe cha bati (Aluminium) kimoja.

*NB: Vyombo vya plastic haviruhusiwi kabisa.*

## MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI.

Mzazi /mlezi unaweza kumpatia mwanao kiasi kidogo cha fedha kulingana na mahitaji yake madogo madogo ya lazima. Haruhusiwi kuja na fedha nyingi na iwapo kuna ulazima wa kumtumia mwanao fedha kwa matumizi yake binafsi tumia njia ya simu ya MHASIBU WA SHULE (0786303541) kwa njia ya M-pesa/Airtel money.

***Angalizo:*** -Mzazi/mlezi huruhusiwi kabisa kutumia akaunti ya shule, mabasi kutuma fedha kwa ajili ya matumizi binafsi ya mwanao.

## MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA KURIPOTI.

- Wakati wa usajili mwanafunzi anatakiwa kuwa na nyaraka zifuatazo kwa ajili ya uthibitisho: -
  - Sare ya shule (full school uniform)
  - Barua yake ya maagizo (joining instruction)
  - Vyeti vyake halisi (originals) na vivuli (photocopies) ya vyeti vya taaluma kidato cha nne (IV) pamoja na leaving certificate (cheti cha kuhitimu kidato cha nne (IV)
  - Cheti cha kuzaliwa halisi na kivuli chake.
  - Fomu ya maelezo binafsi kuhusu histori ya mwanafunzi / mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo, na makosa ya jinai.
  - Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
  - Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu
- Cheti cha daktari (medical Examination form) ambacho kimejazwa vizuri na mganga mkuu wa Hospitali ya serikali na siyo Hospitali binafsi. (kiambatisho C)

***ANGALIZO:***

➢ Nyaraka zilizotajwa hapo juu ni muhimu sana tafadhali njoo nazo bila kukosa.
➢ Utasajiliwa ofisi ya makamu Mkuu wa shule.
➢ Utawasilisha nyaraka zote za fedha ofisi ya mhasibu.

***ONYO!!!***

- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani
- Mwanafunzi haruhusiwi kwenda bwenini kabla ya kukamilisha usajili wake.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi au kitu chochote kinachohusiana na simu, iwapo atakamatwa na simu au kifaa chochote cha simu atanyang'anywa na **KUFUKUZWA SHULE** (hatarejeshewa simu au vifaa hivyo)
- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na chakula cha aina yoyote ile shuleni.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na pasi, heater, kibatari, karabai, mishumaa, radio, camera, television, jiko lolote la kupikia na sufuria, chupa za chai.NI MARUFUKU.
- Mwanafunzi hatakiwi kuchelewa shule kwa tarehe iliyopangwa na iwapo atachelewa kwa muda wa siku saba (7) baada ya tarehe ya mwisho ya kuripoti bila taarifa ya maandishi atakuwa amepoteza nafasi yake.
- Mwanafunzi haruhusiwi kufuga kucha, kuweka kucha za bandia, kope za bandia, kupaka rangi kwenye kucha, lipstick, wanja, kuweka dawa kwenye nywele, kutumia vipodozi na haruhusiwi kufuga nywele, kusuka nywele, hivyo atatakiwa kunyoa nyele zake na ziwe fupi muda wote kwa wastani wa kuchana na kutumia kitana kidogo.
- Mwanafunzi anatakiwa: -kusoma, kuelewa kuzishika na kuzifuata sheria za shule ambazo atafafanuliwa mara tu afikapo shuleni. Baadhi ya sheria hizo zimeambatishwa pamoja na form hii.
- Ni vyema mwanafunzi asindikizwe na mzazi/mlezi wake ili mzazi au mlezi huyo afahamu mazingira ya shule na mahali shule ilipo na vilevile kufahamiana na watumishi wa shule na kuwa na uhakika ya kuwa mtoto wake amefika salama mahali panapostahili.
- Aidha shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na marekebisho yake Na 10 mwaka 1995 vilevile shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

Kwa kifupi mwanafuzi azingatie mambo yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa kina mara tu afikapo shuleni: -

**Mwanafunzi atatakiwa**:

- Kuheshimu viongozi, wazazi, wafanyakazi wote na jamii kwa ujumla.
- Kuhudhuria vizuri shughuli zote za ndani na nje ya darasa au ya shule•
  Kutekeleza kwa makini na kwa uaminifu na uadilifu mkubwa shughuli zote za shule kama ilivyo kwenye ratiba.
- Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine atakazo pangiwa
- Kukimbia mara aitwapo na mtu anayemzidi umri.
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo yote juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wake katika shule hii.
- Kutunza usafi wa mwili na mavazi pamoja na mazingira yote ya shule.
- Kuvaa sare ya shule iliyo ndefu na safi wakati wote anapokuwa ndani au nje ya mipaka ya shule.
- Mwanafunzi haruhusiwi kutembelewa na mzazi au mgeni wake bwenini. (wazazi/walezi wanaruhusiwa kutembelea watoto wao kila Jumapili ya mwisho wa mwezi)
- Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele hata kama anavaa ijabu
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote ambapo ratiba ya shule huanza saa.**11:00 alfajiri kwa mchakamchaka na kuishia saa 4:30 usiku baada ya ukaguzi (Bed checking) ambapo taa zote za ndani ya mabweni na madarasa huzimwa na wanafunzi kulala.**

***MAMBO/MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.***

1. Wizi wa aina yoyote
2. Kokuhudhuria masomo kwa zaiadi ya siku tisini (90) mfululizo.
3. Uasherati, ushoga na usagaji.
4. Ubakaji.
5. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, mirungi, cocaine, mihadarati na kuberi.
6. Kupigana na kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kudharau Bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa, Fedha ya Taifa, wimbo wa Taifa na viongozi wote.
9. Kuoa na kuolewa.
10. Kutoa mimba au kuharibu mimba ukiwa ndani au nje ya shule.
11. Kupata mimba au kusababisha mimba.
12. Kugoma, kuchochea au kuvuruga amani na usalama wa shule na jamii.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Kuwa na kumiliki simu ya mkononi, charger, line ya simu na vifaa vyote vya umeme.
15. Kulala nje ya shule bila taarifa/kutoroka.

Mwisho kwa niaba ya jumuiya ya CHIEF SARWATT sekondari, napenda kukukaribisha sana hapa shuleni na kukutakia safari njema na mafanikio mema katika masomo yako ya kidato cha V na VI.

Kauli mbiu ya shule yetu ni: - **“EDUCATE TO HELP SOCIETY”**

KARIBU SANA CHIEF SARWATT SEKONDARI

R. I. JUMA
MKUU WA SHULE

**A. FOMU NA. 01**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**
**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MBULU TOWN COUNCIL REQUEST FOR**
**MEDICAL EXAMINATION**

**HEADMISTRESS,**
**CHIEF SARWATT SECONDARY SCHOOL,**
**P.O.BOX 42,**
**DATE …….**

**REF. Na.SSS/F05/01/VOL2**
**TO MEDICAL OFFICER,**
**……**
**……**
**……**
**FULL NAME**

**……...**

Please examine the above named pupil as to her fitness for entrance to this school in form V – 2021/2022.

1. Stool Examination ……
2. Blood counter (red and white) ……
3. Urinal analysis ……
4. T.B Test ……
5. Syphilis Test ……
6. Eye Test ……
7. Chest ……
8. Spleen ……
9. Abdomen ……
10. Check cases of pregnancy in girls ……

Additional information e.g. Physical defect or impairment, infection, chronic family diseases etc.
……
……
……
……

**MEDICAL CERTIFICATE**
(To be completed by the medical officer)
I have examined the above and consider that she is physically fit for appointment /engagement as above
Date …… Signature
……. Station …….
Designation …… Note to medical officer at the time of examination
"Please treat individual for an ailment you noted."

********** DELETE AS NECESSARY **********

**B. FOMU NA. 02**

**MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI**

**SEHEMU A** (Ijazwe na mwanafunzi mwenyewe)

1. Jina la mwanafunzi (majina matatu) ……
2. Uraia……
3. Tarehe ya kuzaliwa……
4. Shule anakotoka……
5. Tarehe ya kutoka shule hiyo……

**SEHEMU B: (Ijazwe na mzazi/mlezi)**

1. Jina la mzazi/mlezi (majina matatu) ……
2. Anwani ya mzazi/mlezi ……
3. Mahali anapoishi (Kijiji/Kata) ……
4. Kazi ya mzazi/mlezi……
5. Mahali anapofanya kazi ……
6. Ndugu wawili wa karibu (wanaweza kuwa badala ya mzazi/mlezi)
    a) Jina …….
    Anwani yake ……..
    Uhusiano wake na mwanafunzi……
    Uhusiano wake na mzazi/mlezi……Tarehe……
    Sahihi ya mzazi……
    b) Jina …… Anwani yake ……. Uhusiano wake na mwanafunzi……Uhusiano wake na mzazi/mlezi……Tarehe……. Sahihi ya mzazi……

**C. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.**

**SHULE YA SEKONDARI CHIEF SARWATT,**
**S.L.P 42,**
**MBULU – MANYARA.**
**……**

**MZAZI/MLEZI WA ……**
**YAH: MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE PIA KUSHIRIKIANA NA SHULE KUMLEA MWANAFUNZI**
**(IJAZWE NA MZAZI/MLEZI MWENYEWE)**

1. Jina kamili …….
2. Kazi yake……. Umri……
3. Anwani ya nyumbani…….……
4. Kijiji.....……Kata…….……Tarafa……..……
5. Wilaya…….,….Mkoa……..…….……Uraia…….
6. ( a) Dini ya mzazi/Mlezi…….…….
   (b) Namba ya simu kama ipo……Mji……
7. Dhehebu unalotaka mwanao alelewe……
8. Anwani kamili ya nyumbani ambapo mtoto atakuwa anakwenda wakati wa likizo……..
9. Anwani ya kazini ikiwa inatofautiana na hiyo hapo juu na kila mara inapobadilika tunaomba utuarifu rasmi kwa barua kupitia kwa mkuu wa kituo/Mwenyekiti wa kijiji chako/mwajiri wako……
10. Nimesoma barua ya kuripoti shuleni, sheria za shule na fomu zote zilizoambatishwa. Nimeelewa na kuridhika na ninakubali wajibu huo nikijua ni ahadi ambayo sitaweza kukiuka bila kuhitaji hatua za kisheria zinazostahili kuchukuliwa dhidi yangu.
11. Naahidi wakati wote kushirikiana na kusaidiana na waalimu katika kumlea kijana wangu ili awe natabia njema siku zote, mchapakazi na mwenye bidii ya masomo. Nitatimiza mahitaji yake yote kulingana na miongozo ya shule. Juu ya hayo naelewa mwanangu akienda kinyume na sheria za shule hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Nathibitisha kwamba habari zilitolewa hapo juu ni kamili na ni za kweli Jina la

Mzazi/mlezi……..…….Sahihi……Tarehe……

Jina la Afisa Mtendaji ……Sahihi ya Afisa Mtendaji ……tarehe……

Ndugu/jamaa (3) watatu watakaoruhusiwa kumtembelea mototo/mwanafunzi nje ya wazazi/walezi.

N.B Ndugu na jamaa watakaothibitishwa hawatahusika katika maamuzi ya masuala ya kinidhamu ya mwanafunzi.

Mimi mzazi/mlezi nathibitisha kuwa waliojiandikisha hapo chini ni ndugu zangu/jamaa wa karibu ambao wanaoweza kuruhusiwa kumtembelea mtoto wangu na siyo vinginevyo. Jina la mzazi/mlezi.....Saini.....

| S/N | MAJINA MATATU | UHUSIANO WAKE NA MTOTO | ANWANI | SIMU YA MKONONI | SAHIHI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |

**N.B Sehemu 'B'ijazwe na kusainiwa na mzazi na si vinginevyo**

**SHULE YA SEKONDARI CHIEF SARWATT,**
**S.L.P 42,**
**MBULU – MANYARA.**
**……...**

**KWA MWANAFUNZI ……**

**YAH: MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI (KUWA MTIIFU NA MWENYE NIDHAMU KWA MUDA WOTE AWAPO SHULENI).**

Mimi ……. wa kidato cha tano mwaka 2021/2022. Ninaahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu, Jina…….

a) Nitatii amri zote za CHIEF SARWATT Sekondari pamoja na miongozo mbalimbali ambayo imetolewa na viongozi wa shule kuanzia ngazi ya kiongozi wa darasa(monitor), viranja, wafanyakazi wasio waalimu, waalimu na Mkuu wa shule;
b) Kuwa nitatimiza wajibu wangu ulionileta hapa shuleni ambao ni kusoma.;
c) Kuwa nitahudhuria masomo darasani na mahali pengine popote nitakapohitajika;
d) Kuwa nitakuwa ndani ya mipaka ya Chief Sarwatt Sekondari wakati wote niwapo shuleni labda tu kwa shida maalum na baada ya kupata ruhusa ya kutoka nje, kwa mwalimu wa zamu au mwenye dhamana ya ruhusa.
e) Naahidi kuwa baada ya kuyaelewa yote hapo juu, nitapokea na kutii maagizo, sheria, amri na maelezo ambayo yatatolewa mara kwa mara shuleni. Sitaenda kinyume na ahadi hii. Nikienda kinyume na sheria za Shule hatua kali zichukuliwe dhidi yangu ambayo ni pamoja na kufukuzwa shule.

Jina ……Sahihi ya Mwanafunzi……Tarehe……
Jina la mzazi/mlezi……Sahihi……Tarehe……
Jina la Shahidi……..……Sahihi……..Tarehe……..
Jina na Sahihi ya Makamu Mkuu wa Shule……..……